MULIKA Na. 40(1) 2021 (157-174)

# Asili, Matumizi, na Mtazamo wa Salamu ya "Shikamoo" katika Jamii ya Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili

*Issaya Lupogo*[1]
Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania

*Khamis Mataka*[2]
Taasisi ya Masheikh na Wanazuoni wa Kiislamu Tanzania

*David Kyeu*[3]
Chuo Kikuu cha California, Berkeley

*Martin Mutabazi Mugisha*[4]
Chuo Kikuu cha Rockview, Zambia

**Ikisiri**

*Shikamoo* ni moja ya salamu zinazotumiwa na jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili kusalimiana. Watu mbalimbali katika majukwaa tofautitofauti wamekuwa wakijadiliana kuhusu salamu hiyo endapo inawafaa watumiaji wa lugha ya Kiswahili au la. Makala haya yanajadili asili, matumizi, na mtazamo wa shikamoo wa jamii mbalimbali zinazotumia Kiswahili. Data za makala haya zimetokana na njia nne: upitiaji wa nyaraka, hojaji, usaili, na ushuhudiaji. Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano (EM) imetumika kuongoza utafiti huu. Matokeo ya makala haya yanabainisha kwamba asili ya neno *shikamoo* ni: "nashika miguu" ambayo inaweza kuwa na fasili kuwa "nipo chini ya miguu yako". Asili hii ya neno shikamoo inanasibishwa na utumwa na ukoloni; inatajwa kuwa ni salamu iliyotumiwa na watwana kuwasalimia mabwana wao wakati wa ukoloni. Matumizi ya salamu hii kwa sasa kama ambavyo imebainishwa pia katika miongozo ya Kiswahili sanifu, ni salamu ya heshima kutoka kwa mtu mdogo kiumri kwenda kwa mkubwa. Aidha, utafiti huu umebaini kwamba 51% ya

[1] **Baruapepe:** *islupgo@mzumbe.a.tz/lupogoissaya1@gmail.com*

[2] **Baruapepe:** *sg@islamicscholars.or.tz*

[3] **Baruapepe:** *kyeu@berkeley.edu*

[4] **Baruapepe:** *mugmartino@gmail.com*

watumiaji wa lugha ya Kiswahili walioshiriki katika kujaza hojaji walidai salamu ya shikamoo ni nzuri wakati 30% walisema kuwa salamu hiyo ni mbaya kwa sababu ina asili ya utumwa/ukoloni na 19% walitoa majibu mengine yakiwemo kuiona salamu hiyo ina mapokeo mazuri na mabaya miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili. Makala yanatoa rai kwamba ijapokuwa watu wengi wanapendezwa na salamu ya *shikamoo*, hatutakiwi kupuuza mawazo ya wale wanaoona salamu hiyo si nzuri; hivyo, inapendekezwa kwamba salamu hiyo isilazimishwe bali watu waitumie kwa hiari yao.

## 1.0 Utangulizi

Salamu ni utamaduni uliojengeka duniani kote. Suala la kusalimiana miongoni mwa watu lina maana au linafanya kazi mbalimbali: mathalani, ni sehemu ya kutambulisha uhusiano baina ya watu; kudumuisha uhusiano uliopo baina ya watu; njia ya kuonesha hali ya upole, uungwana na tabia njema kwa mwenzako; na wakati mwingine hali ya kuonesha kuthaminiana (Schegloff, 1968, Brown, 1980 na Yahya-Othman, 1995).

Watu husalimiana kwa namna mbalimbali kama vile kwa kushikana mikono, kuinamisha vichwa, kubusiana, kukumbatiana, kwa kutumia maneno mbalimbali n.k. Mara nyingi hali hizo zilizobainishwa huambatana na maneno fulani ya salamu. Katika baadhi ya nchi za Ulaya, upo utamaduni wa kubusu mkono wa mwanamke mwenye heshima. Katika nchi za Kituruki, Brunei, Indonesia na Ufilipino kuna utamaduni wa kubusu mkono wa mkubwa ikiwa ni ishara ya heshima kwake. Aidha, hata Tanzania zipo jamii kama vile Wahehe wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wana mazoea hayo ya kubusiana mikono tena kwa muda mrefu kidogo kama ishara ya heshima na mapenzi baina yao; salamu hiyo haizingatii rika au/na jinsi fulani tu bali hutumika kwa ujumla. Aidha, katika taasisi ya kama vile Kanisa Katoliki, kuna mazoea ya kubusu pete za wakuu wa kanisa hilo kama ambavyo baadhi ya maeneo waumini wa dini ya Kiislamu wanavyobusu mikono ya mashehe na masharifu wao. Kwa jamii za Kiarabu, pua kugusana na mikono ni miongoni mwa matendo ya kuonesha heshima kutoka kwa mdogo kwenda kwa mkubwa na kwa wale wa rika moja ishara hiyo hutumika kusalimiana. Kwa baadhi ya jamii za Tanzania pia, mtu akitaka kumsalimu mwingine au kumpa kitu ni lazima apige magoti au achuchumae mbele yake. Utamaduni huu wa kupiga magoti nchini Tanzania ni maarufu kwa jamii za Wayao, Wasukuma na Wahehe miongoni mwa jamii nyinginezo.

Kama inavyoelezwa na Mapunda na Sommer (2017) (ijapokuwa katika makala yao walilenga jamii moja tu ya Wangoni) kwamba mabadiliko ya salamu yanasababishwa na umri, jinsi, mahusiano baina ya wazungumzaji, tukio la mazungumzo na mahali ambapo mazungumzo yanapofanyika.

*Shikamoo* ni moja ya salamu zinazotumiwa na jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Salamu nyingine zinazotumiwa na jamii ya watumiaji wa lugha ya

Kiswahili habari za leo/jana/siku/asubuhi/mchana, mambo, unaendeleaje, umeshindaje, Bwana Yesu asifiwe, Tumsifu Yesu Kristo, salaam aleikum, na ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, n.k. Watu mbalimbali katika majukwaa tofautitofauti wamekuwa wakijadiliana kuhusu salamu ya "shikamoo" endapo inawafaa watumiaji wa lugha ya Kiswahili au la. Salamu ya "shikamoo" imewahi kufanyiwa tafiti na Mapunda na Sommer(2017) katika kabila la Wangoni linalopatikana Kusini mwa Tanzania katika mkoa wa Ruvuma. Wao walichunguza ni wakati na mazingira gani salamu ya *shikamoo mama/baba* inachukua nafasi ya *tukuwoni mawu/dadi* katika salamu za kabila la Wangoni. Matokeo yalibainisha kwamba lugha ya Kingoni inayozungumzwa na vijana (miaka 15-30) imeathiriwa sana na Kiswahili; hivyo, ilibainika kwamba wao (vijana) hutumia zaidi *shikamoo* (anayesalimiwa anaitikia *marahaba*) wanapowasalimia wakubwa wakati wazee (zaidi ya miaka 50) hawatumii *shikamoo* kusalimia wazee wenzao waliowazidi umri bali hutumia *tukuwoni* (anayesalimiwa anaitikia *yewo*). Tafsiri ya *tukuwoni* na *yewo* ni habari na nzuri mtawalia.

Aidha, William (2018) alitazama matumizi ya *shikamoo* katika mtandao wa kijamii uitwao *Jamii Forums* akilenga jinsi neno hili linavyotumika katika mikatadha mbalimbali inayoonesha matumizi ya maana ya msingi na matumizi ya maana ya ziada. Hii inaweza kutafsiriwa kwamba matumizi mengine ya *shikamoo* yalikuwa ni ya kimsimu ijapokuwa mwandishi hakuligusia suala hilo moja kwa moja. Yeye alibaini kwamba *shikamoo* hutumika kwa ajili ya kutimiza malengo nane: kusalimiana, kuonesha heshima, kupongeza, kusifu, kusalimu amri, kukejeli, kuomba, na kukataa. Utafiti wa William unajielekeza kujadili *shikamoo* katika matumizi yake mapana kama ambavyo inatumika katika mitandao ya kijamii, na matumizi mengi yakiwa ni maana za ziada za neno hilo katika miktadha isiyo rasmi. Makala haya ya kwetu sasa yamemakinikia *shikamoo* kwa maana ile ya msingi (salamu) hususani kuangalia asili, mapokeo na mtazamo wa watu kuhusu salamu hiyo.

Salamu ya *shikamoo* inaonekana kuwa na mjadala mkubwa miongoni mwa watumiaji, wadau, na wanazuoni wa Kiswahili. Maswali ambayo mara nyingi yamekuwa yakiibuka na bado hayajaandikiwa au kutafitiwa ni: nini asili ya neno "shikamoo"? Shikamoo inatumikaje katika jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili? Je, salamu hiyo ni nzuri au mbaya? Kwa kuwa bado hakuna andiko wala utafiti uliojadili masuala haya yaliyoulizwa kwa utoshelevu, makala haya yanajielekeza kuibua mjadala wa masuala hayo na hatimaye kutoa hitimisho na mapendekezo kutokana na data zilizokusanywa na kuchanganuliwa kwa kuongozwa na kiunzi cha nadharia husika.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yanaongozwa na Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano (kuanzia sasa EM). EM ni nadharia iliyoasisiwa na Dell Hymes mwaka 1972, kisha akaishadidia tena katika maandiko mengine mawili; andiko la mwaka 1974 na

andiko la mwaka 1975. Huyu ni mwanaanthropolojia kutoka Marekani. Hymes pia alikuwa mwanaisimu na mtaalamu wa Sanaajadiia. Tangu kuchipuka kwake katika miaka ya 60, nadharia hii imetumiwa sana na wataalamu katika maeneo mbalimbali ya kiakademia na kitaaluma. Mwanzoni, Hymes (1972) aliita nadharia hii "ethnografia ya mazungumzo", ila baadaye aligundua kwamba mazungumzo na mawasiliano ni dhana mbili ambazo zinakaribiana kwa uamilifu wake, mawasiliano yakiwa jumuishi zaidi ya mazungumzo.

EM ni mwegemeo jumuishi wa utafiti unaotumia misingi ya kiethnografia kuchanganua mawasiliano yoyote yale, pamoja na kuchunguza mazingira yanamotokea. Nadharia hii hufanya hivi ili kutambua mazingira halisi ya kitamaduni na kimuktadha ambamo mawasiliano hutokea. EM hutoa misingi thabiti ya kinadharia na mbinu inayoweza kutumika katika kuchanganua matini zinazotokana na mawasiliano ya watu wanapotangamana. EM inahusika na uchanganuzi wa viambajengo vya mawasiliano kama vile washiriki kwenye mawasiliano, mazingira, muktadha na njia wanazotumia washiriki ili kufanikisha mawasiliano.

Kihistoria, EM ilizuka kutokana na ombwe lililokuwapo katika isimu inayoegemea nadharia za lugha na mbinu za uchanganuzi wa lugha zilizoasisiwa na Chomsky. Itikadi ya Chomsky, ilitilia mkazo zaidi masuala-bia ya kidhahania (ya kiakili na king'amuzi), katika kutoa maelezo kuhusu lugha. Kwa upande mwingine, kuzuka kwa EM pia kulichochewa na pengo lililoachwa na maandiko yake Saussure yaliyotilia sana mkazo muundo na kanuni za lugha. Upungufu wa miegemeo ya Chomsky na Saussure ulisababisha kuzuka kwa EM iliyokuwa na nia ya kuvuruga taratibu maalumu na 'za kistaarabu' zilizoshikiliwa na Chomsky na Saussure katika kuchanganua lugha. Kwa kiwango fulani, mwasisi wa EM, Hymes, na walioendelea kuipigia nadharia hii chapuo baadaye walichukulia kwamba mawasiliano si 'hisabati', na kwamba kuna mambo mengine yanayotokea katika mawasiliano, ambayo hayakutiliwa maanani.

Hymes aliongezea kwa kudai kwamba mwingiliano uliopo kati ya lugha na masuala ya kijamii unatokana na hali kwamba dhima ya lugha ni kufanikisha desturi za kitamaduni zilizopo katika jamii. Mawazo ya Hymes yalidhihirika kwa mara ya kwanza katika chapisho lililoitwa *Antropolojia na Tabia ya Binadamu*, lililoalika michango ya makala kutoka wataalamu wengine pia. Kwenye chapisho hilo, mtazamo wake Hymes kuhusu dhana "mazungumzo" ulikuwa tofauti kidogo, hali iliyosababisha kubadilishwa kwake na kuwa "mawasiliano", neno ambalo lilionekana kuwa jumuishi zaidi. Hymes aliiona dhana jumuishi ya "mawasiliano" kama iliyojumuisha hulka mseto za binadamu anapotoa matamshi yake.

Kwa mujibu wa Hymes, binadamu hajifunzi tu tabia kupitia lugha, bali pia binadamu hudhihirisha tabia yake kupitia lugha anayotumia. Katika tukio la kimazungumzo, yapo matumizi halisi ya kiisimu na ya kimawasiliano 'parole', ambayo ni tofauti na ya kidhahania 'langue', ambayo yanazingatia misimbo ya kiisimu zaidi, badala ya jinsi ambavyo misimbo hiyo huibuliwa katika shughuli

nzima ya mawasiliano. Hymes alitambua kwamba ethnografia ya mazungumzo inashughulika na hali mbalimbali za mazungumzo kama tukio linalojitosheleza, hali mojawapo ikiwa uamilifu wake. Baadaye, Hymes aliendeleza mtazamo huu kwa kuzua ruwaza mahususi iliyotumiwa kuelezea mazungumzo katika aina mbalimbali za mawasiliano.

Tangu miaka ya 80, EM imetumiwa kwa ufanisi mkubwa katika uchanganuzi wa mawasiliano kupitia kazi za Philipsen (1987) pamoja na wanafunzi wake, na machapisho yaliyozuka baadaye katika lugha na sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kazi hizi zimepanua EM, msisitizo ukiwa kwenye msimbo unaotumika katika mawasiliano, na matumizi ya njia za kisayansi katika kuchunguza mawasiliano. Makala haya ni jaribio la kuendelea kupanua utafiti wa mawasiliano katika lugha ya Kiswahili kisayansi na kibinadamu, hususani kwa kuchunguza maamkizi ya "Shikamoo". Kwa hiyo, makala haya yanamakinikia kutazama jinsi jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili inavyotumia lugha yao hususani wanavyotumia salamu ya “shikamoo”.

## 3.0 Methodolojia

Utafiti huu ulihusisha ukusanyaji wa data kutoka katika vyanzo mbalimbali kuhusu asili, matumizi, na mtazamo wa salamu ya shikamoo miongoni wa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Data zilikusanywa kutoka kwa watu mbalimbali ambao ni sehemu ya jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla njia nne zilitumika kukusanya data kwa ajili ya makala haya. Njia ya kwanza ni upitiaji wa nyaraka mbalimbali zinazoonesha maana na etimolojia ya neno *shikamoo* ambapo kamusi mbalimbali za Kiswahili sanifu zinatoa maana yake, ila si etimolojia. Njia ya pili ni ushushudiaji; baadhi ya data zilikusanywa kwa kutazama jinsi salamu hii inavyotumiwa na watu ndani ya jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Data kwa njia ya ushuhudiaji zilikusanywa nchini Tanzania, Kenya, na Lusaka nchini Zambia, ambako Kiswahili kinatumika. Sehemu hizo zilichaguliwa kinasibu tu kama sehemu changamani zinazoweza kuwakilisha sehemu nyingine nyingi ambazo zina watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Njia ya tatu ni hojaji; maswali mbalimbali yaliandaliwa kwa mfumo wa *google docs* yaliyohusu salamu ya *shikamoo* na kutumwa kwa jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili kwa njia ya mtandao ili kujua ni jinsi gani wao wanatumia salamu hiyo na mtazamo wao kwa ujumla kuhusu salamu hiyo. Fomu hiyo ya kimtandao ilisambazwa kwa watumiaji wa Kiswahili kwa kutumia jamvi la WhatsApp la Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU). Data kwa njia hii ilikusanywa kutoka kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili hamsini na watatu (53) kutoka katika jamii thelanini na moja (31). Jamii hizo ni: Wasambaa, Wakamba, Wachaga, Wanyakyusa, Wakinga, Wanyaturu, Wakalenjini, Wamambwe, Wanyam wanga, Wanyambo, Wasukuma, Wakurya, Waluyia-Maragoli, Waha, Wapunjabi, Wamuha, Wajita, Wagogo, Wasagala, Wahehe, Wapangwa, Wanyamwezi, Wapare, Wahaya, Wapemba, Wanyiramba, Wasagari,

Waafro-Arabs, Wanyiha, Wanande, na Wangoni. Idadi hiyo ya watu na jamii ndiyo iliyojitokeza kujaza hojaji yetu.

Njia ya nne ni usaili ambapo watu wawili ambao waandishi wa makala haya waliowaona ni kati ya wataalamu wenye hazina ya historia ya lugha ya Kiswahili waliwasaili na kupata mawazo yao kuhusu salamu ya *shikamoo*. Njia ya usampulishaji lengwa ilitumika kuwachagua watalaamu hao wawili ambapo sababu iliyotumika ni kuchunguza umahiri na weledi wao katika kuifahamu lugha ya Kiswahili hususani historia yake. Uteuzi wa watu hao ulifanyika kwa kuzingatia maandiko yao mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na kufuatilia uchambuzi wao wa masuala ya lugha ya Kiswahili katika majukwaa mbalimali vikiwamo vyombo vya habari.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yanawasilishwa kwa msingi wa masuala matatu: asili ya *shikamoo*, matumizi ya *shikamoo*, na mtazamo wa *shikamoo* katika jamii za watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

### 4.1 Asili ya Neno *Shikamoo*

Kwa kutumia njia ya usaili, mmoja wa wataalamu wa Kiswahili aliyesailiwa, anaeleza kwamba asili ya neno *shikamoo* kwa kutumia vyanzo mbalimbali pamoja na tajiriba yake. Anaanza kwa kulitazama neno kuwa asili yake ni lahaja ya Kimvita cha kale. Anabainisha kwamba katika lahaja hiyo, salamu hiyo ilikuwa inatamkwa: 'nakushika moo'. Katika Kimvita cha kale na katika lahaja nyinginezo za Pwani ya Kenya, "moo" maana ya ni miguu au *maguu* kwa Kimvita cha leo. Kwa hivyo, kwa tamko hilo, mdogo humwambia mkubwa wakati wa kumwamkia kwamba jinsi nikuheshimuvyo, 'nakushika miguu yako'. Aidha, hapo kale, aliyekuwa akiamkia, hakuamkia kwa maneno tu bali aliinama na kushika miguu ya yule aliyemwamkia.

Pia, mtaalamu huyu alikuwa akirejelea utungo wa Takhamisa ya Liyongo, iliyotungwa na Sayyid Abdallah Ali bin Nassir (1720-1820), mtunzi wa ule utunzi maarufu wa Inkishafi. Katika Takhamisa hiyo, neno "moo" limetumika pale Fumo Liyongo alipokuwa amekamatwa na kufungwa pingu. Akiwa kifungoni, akawa akikumbuka ushujaa wake kabla ya kukamatwa, na akawa anasikitika kwamba sasa miguu yake imefungwa pingu, na shingoni mwake amefungwa chuma. Mfano, katika ubeti mmojawapo kuna mshororo huu:

> *Ela* **moo** *yangu yoo mawili kuwa p'inguni,*
> *na shingoni mwangu niweshiwe peto la chuma.*
> [Tafsiri: Bali miguu yangu miwili kufungwa pingu
> na shingoni mwangu kuvishwa mkunjo wa chuma]

Mtaalamu huyu pia alirejelea namna neno *moo* lilivyotumika katika shughuli za harusi ya Kiswahili likiwa na maana ya 'miguu'. Miongoni mwa ada afanyiwazo

bwana harusi ni sherehe ya kuoshwa miguu. Ada hiyo huitwa 'kuosha moo'. Hii hufanyika Unguja pia, ambapo uoshwaji uliambatana na nyimbo mbalimbali.

Kwa ujumla, maelezo haya yote yanajaribu kuchimbua usuli wa neno *moo* kuwa lina maana ya miguu. Hivyo, neno 'shikamoo' tangu kale lilikuwa likimaanisha 'ninakushika moo' yaani 'ninakushika miguu'. Kama inavyofahamika kwamba miguu ni sehemu ya mwili wa mwanadamu ambayo hutumika kutembelea kila mahali. Aghalabu, sehemu hii ya mwili huwa na uchafu au walau hisia za kuwapo uchafu. Pamoja na kufahamu yote hayo lakini anatokea mtu anashika miguu hiyo ama kwa kuomba radhi au kuonesha heshima bila kujali sifa za miguu, zikiwamo zilizodokezwa hapo juu.

Asili ya neno *shikamoo* imetolewa pia katika data za hojaji. Zifuatazo ni nukuu kutoka katika hojaji zinazoonesha asili ya neno hilo:

*….tafiti na baadhi ya wakongwe wao husema ilitumika wakati wa ukoloni kuonesha heshima kuu kwa mkoloni; kwa hiyo, Mwafrika kweli aliashiria salamu kwa kushika sehemu ya nyuma ya mguu wake kuashiria anamheshimu mkoloni. Kwangu naona ni dhuluma kwa sababu salamu ni itikadi kwa Waafrika ila huwa ni kwa hiari. Hii ni zaidi ya heshima ya mapenzi na si heshima ya ukoloni au ya lazima.*

Tofauti na mtoataarifa mwingine ambaye aliandika hivi:

*Naelewa kuwa neno shikamoo kwa kiarabu lina maana nipo chini ya miguu yako; kama nilivyosema hapo awali, kiujumla tumelichukua kama ni salaam ya heshima; kwa hiyo, iendelee tu. Asante.*

Mtoa taarifa mwingine aliandika hivi:

*Hapa naweza kusema neno shikamoo wakati mwingine inaonekana kuwa ni neno la ajabu mfano kuna mwalimu mmoja kanifundisha kidato cha pili alikuwa hataki kuambiwa shikamo bali umwambie heshima yako mwalimu. Mtu akikusalimia shikamoo imezoeleka kuwa ni salamu ya kuonesha mkubwa lakini sivyo kwani neno shikamo ni kama shika moyo wako au niko chini ya miguu yako ambayo siyo haki hata kidogo.*

Kwa hiyo, maelezo ya mtaalamu aliyetajwa hapo juu yakiunganishwa na maelezo ya watoataarifa wa hojaji yanaonesha wazi kwamba asili ya neno *shikamoo* ni ufupisho wa sentensi "*nashika miguu yako*". Ingawa maelezo ya watoataarifa wa hojaji yanadai kuwa hiyo ni salamu ya kikoloni, yanaonesha kukosa ithibati ya kitaalamu kwa sababu hatujui waliojibu ni weledi gani kielimu hususani katika kuijua lugha ya Kiswahili. Ni rahisi kuhusisha salamu hiyo na madai ya watoataarifa wa hojaji hasa ukijikita kuchunguza jinsi ya salamu yenyewe inavyochakatwa kama ambavyo mtaalamu tuliyemfanyia usaili ameeleza.

Miongozo mbalimbali ya Kiswahili sanifu imetoa fasili ya neno shikamoo kama ifuatavyo: TUKI (2014), wanaeleza kuwa shikamoo ni salamu ya heshima itolewayo kwa mtu aliyekuzidi umri. Aidha, kwa mujibu wa BAKITA (2015) shikamoo ni tamko la heshima linalotumika katika maamkizi ambapo mtu mwenye umri mdogo humwambia mtu mwenye umri mkubwa (asili yake ni Kiarabu). Nao BAKIZA (2010), wanafafanua kuwa shikamoo ni maamkizi ya heshima ya mtu kwa mwingine aliyemzidi umri.

Kwa ujumla, maudhui jumuishi kuhusu neno *shikamoo* kutoka kwa wataalamu hao yanatupa ujumbe ufuatao: mosi, shikamoo ni tamko la heshima. Pili, tamko hili la heshima hutolewa na mtu mwenye umri mdogo kwenda kwa yule mwenye umri mkubwa. Kwa hiyo, tunaweza kusema kwamba kigezo cha mtu kutoa au kupewa na kupokea shikamoo kwa mujibu wa wataalamu hao ni umri tu.

Aidha, kupitia data kwa njia ya ushuhudiaji, utafiti wetu umebaini pamoja na mambo mengine kwamba, *shikamoo* pia huweza kuambatana na vionjo vingine kama kushikana mikono, wakati mwingine kushika kichwa cha anayeamkiwa, kubusiana kwenye viganja vya mikono, n.k.

Kwa hiyo, kwa ujumla asili ya neno *shikamoo* ni ufupisho wa sentensi "nashika miguu yako". Kwa kuzingatia maana zilizotolewa katika kamusi mbalimbali, kwa sasa neno hilo lina maana ya salamu ya heshima inayotolewa kutoka kwa mtu mdogo kiumri na kwenda kwa mtu mkubwa kiumri. Lakini ukijikita kuhusisha asili ya neno lenyewe ambayo ni "nashika miguu yako" au "niko chini ya miguu yako", na kwa kuzingatia majibu ya hojaji yanayogusia suala hilo, ni bayana kwamba salamu hiyo kiasili pia inanasibishwa na ukoloni. Inaonekana ni salamu iliyotumiwa na watwana kuwasalimu mabwana zao kwa heshima iliyopitiliza: "niko chini ya miguu yako/ninashika miguu yako".

### 4.2 Matumizi ya S*hikamoo* katika Jamii za Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili

Tukianza na data kutoka katika hojaji, watoataarifa walihojiwa hivi: "Tunaomba utueleze kwa kifupi muktadha ambao wewe binafsi unatumia (kumsalimia mtu au kusalimiwa na mtu) *shikamoo.*" Nukuu zifuatazo zinabainisha matumizi ya *shikamoo* miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni majibu ya swali hili:

Mmojawapo aliandika hivi:

*Shikamoo naitumia kwa mtu aliyenizidi umi au cheo*

Mwingine alijibu hivi:

*Ninasalimiwa SHIKAMO na watu walionizidi umri. Nami nasalimu SHIKAMOO kwa watu walionizidi umri. Walionizidi mali na madaraka kama ni wadogo wangu kwa umri siwapi SHIKAMOO.*

Mtoataarifa mwingine alijibu hivi:

*Shikamoo ninamsalimia anayenizidi umri, kusalimiwa inategemea kipimo cha mtoa salamu , kwangu jukumu ni kupokea au kuitikia.*

Kwa ujumla, majibu kutoka katika hojaji yanaonesha kwamba salamu hii hutumika kumsalimia mtu aliyekuzidi umri, cheo au mali.

Mtaalamu wa pili aliyesailiwa alibainisha kwamba *shikamoo* kwa ujumla, ni neno linaloonesha heshima kutoka kwa mtoto kwenda kwa mkubwa.

Kwa kiasi kikubwa hata kupitia ushuhudiaji wa namna watumiaji wengi wa Kiswahili wanavyotumia lugha hiyo kwa msingi wa mtu mwenye umri mdogo kumsalimia *shikamoo* mtu aliyemzidi umri, anayesalimiwa hujibu *marahaba*.

Kwa hiyo, matumizi ya *shikamoo* kwa kiasi kikubwa yanafanana miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili; ni salamu inayohusisha mtu mwenye umri mdogo kumsalimia mwenye umri mkubwa. Vilevile, wakati mwingine inahusisha asiye na cheo (mwenye cheo kidogo) kumsalimia mwenye cheo (cheo kikubwa). Pia, kama ilivyobainishwa katika hojaji, wakati mwingine (ijapokuwa si kwa watu wengi) hutumika kumsalimia mtu aliyekuzidi uwezo wa kiuchumi.

Kwa upande mwingine, yapo mawazo tofauti kiasi kuhusiana na matumizi ya *shikamoo*. Yafuatayo ni majibu ya baadhi ya waliojaza hojaji ambayo yanaonesha masuala ya ziada kuhusu matumizi ya shikamoo. Mfano, mmoja aliandika hivi:

*Hapa naweza sema neno shikamoo wakati mwingine linaonekana kuwa ni neno la ajabu mfano kuna mwalimu mmoja kanifundisha kidato cha pili alikuwa hataki kuambiwa shikamo bali umwambie heshima yako mwalimu …mtu akikusalimia shikamo imezoeleka kuwa ni salamu ya kuonesha mkubwa lakini sivyo kwani neno shikamo ni kama shika moyo wako au niko chini ya miguu yako ambayo siyo haki hata kidogo*

Hii inaonesha wazi kwamba lipo kundi la watu ambao hawapendezwi na salamu hiyo ya *shikamoo*. Maelezo haya ya mtafitiwa kutoka katika hojaji yanalandana na ushuhudiaji uliofanywa Zambia (Lusaka) ambapo wengi wao hawakitumii Kiswahili kwa kusalimiana. Wanaanza na salamu ya Kinyanja au Kibemba (lugha za Zambia ambazo zinatumiwa sana Lusaka) kisha wanaendelea na maongezi katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, kupitia ushuhudiaji, ilibainika kwamba kuna baadhi ya watu hutumia salamu za kiimani pekee na wengine walikuwa wakichanganya salamu za kiimani na *shikamoo*. Mathalani, wapo baadhi bila kujali tofauti za umri wanasalima tu *salaam aleikum* (kwa Waislamu) na *tumsifu Yesu Kristo* au *Bwana Yesu asifiwe* (kwa

Wakristo). Lakini kuna wakati mwingine, watu wengine huchanganya salamu hizo, yaani wanaanza na *salaam aleikum* au tumsifu Yesu Kristo, halafu, kama aliyeanza kusalimia ana umri mdogo anamalizia na salamu ya *shikamoo.* Suala hili linashadadidiwa na majibu kutoka kwa watoataarifawaliojibu kupitia hojaji kama ambavyo mmoja aliandika:

*Mimi ninazo salamu mbili, kwa wanafamilia tunatumia salamu ya kidini (salam aleikum ) ambayo haijalishi mkubwa kwa mdogo au mdogo kwa mkubwa na shikamoo kwa watu wa nje ya familia ambao hatuna udugu au ukaribu wa kufahamiana. Aidha, kwa ndugu salamu ni ile ile ya kidini.*

Hii inaonesha mtoataarifa huyu na familia yake wanaitumia salamu ya *shikamoo* na salamu za kidini katika miktadha tofautofauti. Katika familia yao, wanatumia salamu ya kidini wakati wanapokutana watu ambao si wanafamilia, wanatumia *shikamoo* katika misingi ileile ya kuzingatia umri mdogo (anasalimia) na umri mkubwa (anasalimiwa). Katika ushuhudiaji, jambo lingine lililobainika ni kwamba baadhi ya watu wakiwakuta watu ambao ni wadogo kiumri ukilinganisha na wao, endapo wadogo hao kiumri hawajawasalimia *shikamoo*, wakubwa hao huanza kwa kuwasalimia wadogo hao "*hujambo*!". Mategemeo yao wakiwasalimia hivyo, wadogo hao kiumri kuitikia hivi: "*hatujambo*" na kisha kusalimia "*shikamoo*!", kisha wakubwa hao wanaitikia "*marahaba*".

Kwa hiyo, kwa msingi wa uchambuzi kwa kutumia Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano, hii inaonesha kwamba kuna mazingira mengine hasa nchini Tanzania, baadhi ya watu wanaidai *shikamoo* kwa nguvu hata kama mtu hayupo tayari kusalimia kwa salamu hiyo. Hii ni kutokana na sababu kwamba kwa muktadha wa Kitanzania, inachukuliwa kwamba mtu mdogo kiumri anaposalimiwa na mkubwa "hujambo!", ni kawaida kwamba mkubwa huyo anataka kusalimiwa *shikamoo.*

Aidha, kupitia ushuhudiaji na hojaji, imebainika kwamba pamoja na matumizi ya *shikamoo* na salamu za kidini, zipo salamu nyingine kama vile: *habari za asubuhi, habari za mchana, habari za siku, habari za usiku, mambo, mzima, unaendeleaje, niaje* (si rasmi)*, inakuwaje* (si rasmi)*,* na *vipi mishe* (si rasmi).

Kwa hiyo, ijapokuwa kwa kiasi kikubwa inaonekana kwamba salamu ya *shikamoo* hutumika katika miktadha mitatu: salamu ya mdogo kiumri kumsalimia mkubwa kiumri, salamu ambayo mtu anamsalimia mtu aliyemzidi cheo kazini, na wakati mwingine hata kwa mtu aliyemzidi mwenzake kiuchumi/kimali; kwa kiasi fulani, salamu hiyo haina mapokeo mazuri kwa baadhi ya watu.

### 4.3 Mtazamo wa Watu kuhusu Salamu ya *Shikamoo*

Aidha, kutoka katika hojaji, imebainishwa kwamba kati ya sampuli ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili hamsini na watatu (53) walijaza hojaji kutoa mtazamo wao kuhusu salamu ya shikamoo. Swali husika kwa watoataarifa hao lilikuwa likihoji hivi: "Je, una mtazamo gani kuhusu matumizi ya salamu ya shikamoo ndani ya jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili? Salamu hiyo ni nzuri au mbaya? Kwa nini?" Majedwali Na. 1, 2 na 3 yanaonesha majibu waliyotoa watoataarifa kutoka katika hojaji ambapo majibu yao yalikuwa ya namna tatu: shikamaoo ni zuri, shikamoo ni mbaya, na majibu mengineyo mtawalia.

**Jedwali Na. 1: Shikamoo ni Nzuri**

| Na. | Jibu laoataarifa |
|---|---|
| 1. | Hii ni salamu ya unyenyekevu uliochanganyika na woga . Inatumiiwa kwa hofu. |
| 2. | Mimi sidhani kama ni mbaya, kwa sababu kwenye jamii yetu tumeikubali kuwa heshima kwa mtu aliyekuzidi umri. Kwa hiyo, iendelee tu kutumika. |
| 3. | Kwa Waswahili nadhani ni utamaduni. Inabidi iendelee ilivyo. Sina tatizo nalo. Tatizo lililopo ni ikiwa hatupishani umri sana basi nasita kukubali salamu hiyo. |
| 4. | Kwangu naona ni nzuri kwa sababu imebeba thamani ya utu ndani yake mtu kukwambia 'shikamoo' ina mana ametambua wewe ni mkubwa kuliko yeye hasa kiumri. |
| 5. | Ni nzuri ila maeneo fulani tu (hasa pwani) ya Kenya ninamotoka. Kenya bara ni muhali kuisikia ikitumika. |
| 6. | Ni nzuri |
| 7. | Ni nzuri |
| 8. | Nzuri |
| 9. | Ni nzuri, maana bila kuzingatia maana asilia ya neno hilo; inadhihirisha heshima. Katika jamii nyingi za Kiluhya watu hushika mkono wa kulia wanapowasalimia wakubwa wao kama ishara ya heshima. |
| 10. | Ni nzuri sana |
| 11. | Nzuri kwa sababu imezoeleka katika jamii ya Waswahili. |
| 12. | Watoto hufundishwa kunena neno hili na hufurahi kulitumia mbele ya kila mtu wakikutana naye. Hivi karibuni nimegundua matumizi ya neno kama kinga dhidi ya watu wenye nia chafu wa jinsia tofauti. Salamu hii ni nzuri kwa ujumla. |
| 13. | Kimsingi ni nzuri. Ni ya heshima. |
| 14. | Ni nzuri kwa maana ya nipo chini ya miguu yako. |
| 15. | Salamu ni nzuri, kwa kuwa inaweka utii au heshima kwa mtu mwenye umri mdogo kumwamkia mtu mwenye umri mkubwa. |
| 16. | Inategemea na makuzi ya mtu katika jamii husika. *Shikamoo* ni ishara ya heshima na haiathiri mahusiano baina ya watu. Pia, hutolewa kwa ridhaa ya mtu na si kulazimishwa, Hivyo, ni salamu nzuri ambayo inakumbusha wahusika mipaka ya mahusiano yao. |
| 17. | Naona ni salamu tuliyoipokea, sioni ubaya wake kwani hata jamii inaitumia |

| | |
|---|---|
| | pasipo na ubaya wowote. |
| 18. | Kwa mtazamo wangu, salamu hiyo ni nzuri kwa sababu ni kuonyesha heshima kwa wanaokuzidi umri. |
| 19. | Ni salamu nzuri kwa sababu inajenga taswira ya heshima kwa jamii, na pia inasaidia kuondoa utitiri wa salamu kama ilivyo kwa makabila mengine. |
| 20. | Nzuri, kwa sababu humfanya yule unayemusalimu asiwe na wasiwasi wa kukufikiria kuwa umekuja na habari ambazo si mzuri. |
| 21. | Naichukulia kama heshima kwa mtu aliyenizidi umri. |
| 22. | Nzuri |
| 23. | Ni nzuri, kwa sababu inadhihirisha heshima waliyonayo kati ya wasalimianao. |
| 24. | Nzuri, inaonesha heshima kwa anayekuzidi umri. |
| 25. | Nzuri, inaheshimisha. |
| 26. | Matumizi ya shikamoo ndani ya jamii ya Waswahili ni ya heshima sana na ni nzuri kutoka kwa wakubwa kwa wadogo |
| 27. | Ni nzuri, huonyesha heshima ya wadogo kwa wakubwa. |

**Chanzo:** Data za uwandani (2021)

**Jedwali Na. 2: Shikamoo ni Mbaya**

| Na | Jibu la Mtoataarifa |
|---|---|
| 1. | Kwa maana ninayoifahamu ya niko chini ya miguu yako, sio nzuri kwa kua imekaa ya kitumwa na sio ya kutakiana kheri au kujuliana hali. |
| 2. | Mbaya... sababu tafiti na baadhi ya wakongwe wao husema ilitumika wakati wa ukoloni kuonyesha heshima kuu kwa mkoloni, kwa hiyo, Mwafrika kweli aliashiria salamu kwa kushika sehemu ya nyuma ya mguu wake kuashiria anamheshimu mkoloni. Kwangu naona ni dhuluma kwa sababu salamu ni itikadi kwa Waafrika ila huwa ni kwa hiari. Ni zaidi ya heshima ya mapenzi na si heshima ya ukoloni au ya lazima. |
| 3. | Mtazamo wangu neno shikamoo, lisitumike kabisa maana katika mandhari mengine linatafsiriwa kama tusi, salamu hiyo siyo nzuri maana wengi hawaipendi ila wanajilazimu kukubali tu mfano mwalimu darasani inamubidi aitikie pale anapoamukiwa na wanafunzi, ni mbaya kwa sababu haina motisha kwa wanajamii. |
| 4. | Salamu ya shikamoo haifai, kwani haikuwezeshi kujua kama wahusika wanaosalimiana kama wana siha njema ama wanaumwa. |
| 5. | Siiafiki sana japo kwa sababu ya kuishi na jamiii bila kuonekana wa ajabu na lazimika kuitumia sababu najua ni salamu ila sijui maana yake na chanzo chake kwani kuna salamu mbadala na zina heshima tu, mfano kuanza na neno mzee habari za leo, baba/mama habari za nyumbani n.k. |
| 6. | Hii salamu haitofautishi umri/rika hivyo inakosa heshima/uzito fulani, imekaa kibaguzi fulani na kibabe pia |
| 7. | Shikamoo, binafsi naona sio salamu nzuri maana kuna wakati ni vigumu kujua tofauti ya kiumri iliyopo. Pia, imekaa kiujumla zaidi na haitoi Nafasi kwa msalimiaji na msalimiwa kuendelea na mazungumzo zaidi. |

| | |
|---|---|
| 8. | Mbaya kwa sababu haileti uhusiano msawazo katika jamii. |
| 9. | Salamu hiyo si nzuri, kwa sababu salamu hiyo (shikamoo) humaanisha niko chini ya miguu yako. Haina asili ya lugha ya Kiswahili, na inatumika kama salamu. Haina muktadha maalumu, haijulikani ni rejesta ya wapi..., kwa mfano, kanisani watu husalimiana "Bwana Yesu asifiwe, tumsifu Yesu kristo," Msikitini "Assalamu alaikum" lakini neno shikamoo halina rejesta maalumu. |
| 10. | Binafsi neno shikamoo lipo kinyumenyume halina maana kiadili. Shika-kamata mo - miguu nafikiri sasa hauna maana tena kwenye karne huru kama hizi. |
| 11. | Kila kitu vizuri kulengwa kwenye maana kama haina madhara na haiharibu kilichokusudiwa basi sina shida nayo, ila kama maana ni 'ninashika miguu yako' ili iweje? Ukishakuishika…! |
| 12. | Sio nzuri, kwa sababu inamaanisha niko chini ya miguu yako. |
| 13. | Si nzuri , kwa sababu inabeba dhana ya utumwa na utwana kutokana na maana ya neno lenyewe shikamoo: "niko chini ya miguu yako " |
| 14. | Salamu hii inatumika kwa vijana au watoto kuwasalimia watu wazima. Lakini kwa mimi binafsi salam hii kutokana na maana yake naona si nzuri kwenye jamii (niko chini ya miguu yako). |
| 15. | Mbaya |
| 16. | Binafsi nadhani ni mbaya kutokana na historia yake niliyopata kuisikia. Enzi za utumwa Afrika Mashariki, Waarabu walitaka kusalimiwa *"nakushika miguu*" waliposhindwa kutamka wengine wakasema "*shikanukuu"* n.k. Mwisho nyie wataalamu wa lugha ktk kurasimisha/kusanifisha neno husika ili kuwa na neno moja linalotambulika tukaishia kupata neno *shikamoo*. Nashauri kuwa na mbadala wa neno *shikamoo* ktk lugha ya Kiswahili. |

**Chanzo:** Data za uwandani (2021)

**Jedwali Na. 3: Majibu Mengineyo**

| **Na.** | **Jibu la Mtafitiwa** |
|---|---|
| 1. | Kwangu mimi naona inawakanganya watumiaji kwa sababu kwingine inatumika kwingine haitumiki. |
| 2. | Ni salamu iliyozoeleka sana japo fasili yake haifahamiki ipasavyo. |
| 3. | Kwa maana ya kawaida ni salamu anayopewa mtu aliyekusudia umri. Japo mara nyingine inatumiwa kusalimu mtu mwenye pesa bila kujali umri. Zamani walitumia wataanzania kuwasalimu mabwana zao wakimaanisha niko chini ya miguu yako nyakati za utumwa. |
| 4. | Naona ni salamu ya kawaida. |
| 5. | Inategemea. Kama salamu na kujuliana hali haina shida, changamoto ni pale inapowakilisha matabaka ya watu wenye kuheshimiwa zaidi na wenye kuheshimiwa kidogo. Nilitegemea heshima iwe ni kitu kisicho na mpaka wa umri, cheo au nafasi ya mtu. |
| 6. | Ni mazoea tu kwani sisi ambao sio Waswahili tumeikuta hiyo salaam na |

| | |
|---|---|
| | tunaitumia ila chanzo hatukijui. |
| 7. | Najaribu. |
| 8. | Kwa sasa tuiache. |
| 9. | Sioni shida katika salamu hiyo japo natambua kuna watu wanaridhika zaidi wakitumia salamu hiyo na wengine hawaridhiki na salamu hiyo na mara nyingi hutafuta kuikwepa kwa kutumia salamu zingine hasa za itikadi za kidini. Nimebaini pia kuwa hadhi ya salamu ya *shikamoo* hutegemea sana ukanda/eneo fulani. Salamu hiyo kwangu haina shida kwa kuwa imezoeleka, ingawa nahisi kiwango fulani cha utwezaji hadhi, pengine hii ni athari ya lugha mama yangu labda. |
| 10 | "Shikamoo" kwa mtazamo wangu iko kati (mbaya au nzuri) kwa kuwa wengine hawapendi kusalimiwa kwa salamu hii, na wengine wanapenda kwa sababu ina ubaguzi wa umri. |

**Chanzo:** Data za uwandani (2021)


**Jedwali Na. 4: Muhtasari wa Majibu ya Mtazamo wa *Shikamoo***

| **Kategoria za Majibu** | **Idadi ya Waliojibu** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Nzuri | 27 | 51 |
| Mbaya | 16 | 30 |
| Mengineyo | 10 | 19 |
| **Jumla** | **53** | **100** |

**Chanzo:** Data za uwandani (2021)

Baada ya kuona muhtasari wa data kuhusu mitazamo kuhusu salamu ya *shikamoo* kutoka kwa watoataarifa. Muhtasari huo unaweza kuwekwa katika sura nyingine ya mchoro kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.

**Chati Na 1: Mtazamo wa Watoataarifa kuhusu *Shikamoo***




**Chanzo:** Data za uwandani (2021)

Kama ambavyo tumeona, katika kutaka kujua mtazamo watoataarifa kuhusu salamu ya *shikamoo*, watoataarifa 53 (100%) walitoa majibu yao kwa swali husika. Kati yao, watoataarifa 27 (51%) walibainisha kwamba salamu hiyo ni nzuri huku wakitoa sababu mbalimbali zikiwamo: ni salamu ya heshima, salamu iliyozoeleka, na ni salamu ambayo watu wakisalimiwa huridhika. Aidha, watoataarifa 16 (30%) walidai salamu hiyo ni mbaya huku wakibainisha sababu kuu mbili. Sababu ya kwanza ni kwamba salamu hiyo inanasibishwa na ukoloni. Wanadai ni salamu ya kitumwa kwa sababu ilitumika enzi za utumwa ambapo watwana waliwasalimia mabwana wao wakisema *"ninashika migu yako".* Sababu ya pili, salamu hiyo ni ya kimatabaka (umri, uwezo, cheo) tofauti na salamu nyingine za kawaida au za kiimani. Wakati watoataarifa 10 (19%) hawakubainisha moja kwa moja endapo salamu ya shikamoo ni mbaya au nzuri, bali wao walitoa maoni yao mengine mbalimbali kama vile: salamu hiyo ni nzuri na mbaya, salamu hiyo ni ya kawaida, salamu hiyo wanaitumia bila kujua asili yake, n.k.

Uzito wa mawazo ya wanaoona salamu ya *shikamoo* ni mbaya unashadidiwa pia na baadhi ya majibu yaliyowekwa katika kategoria ya "majibu mengineyo"; mathalani, tutazame jibu namba 4 na namba 8 katika Jedwali Na. 3 kama yalivyorudiwa kunukuliwa hapa chini:

*Inategemea. Kama salamu na kujuliana hali haina shida, changamoto ni pale inapowakilisha mataba ya watu wenye kuheshimiwa zaidi na wenye kuheshimiwa kidogo. Nilitegemea heshima iwe ni kitu kisicho na mpaka wa umri, cheo au nafasi ya mtu* (Jedwali Na. 3, jibu la 4)

*Sioni shida katika salamu hiyo japo natambua kuna watu wanaridhika zaidi wakitumia salamu hiyo na wengine hawaridhiki na salamu hiyo na mara nyingi hutafuta kuikwepa kwa kutumia salamu nyingine hasa za itikadi za kidini. Nimebaini pia kuwa hadhi ya salamu ya shikamoo hutegemea sana ukanda/eneo fulani. Salamu hiyo kwangu haina shida kwa kuwa imezoeleka, ingawa nahisi kiwango fulani cha utwezaji hadhi, pengine hii ni athari ya lugha mama yangu labda ((Jedwali Na. 3, jibu la 48)*

Majibu haya kutoka kwa watoataarifa japo hayaoneshi moja kwa moja kwamba salamu hii ni mbaya au nzuri, sehemu za majibu yao inaonesha ni namna gani salamu hiyo ilivyo na mtazamo hasi. Mtazamo hasi wa kwanza ni kwamba salamu hiyo inatengeneza viwango tofauti na salamu nyingine ambazo hazina matabaka. Hili jambo lina mantiki, ni kweli salamu ya *shikamoo* inahusudu matabaka ikilinganishwa na salamu nyingine zilizopo kama vile *habari za asubuhi/mchan/jioni*, salamu za kiimani: *salaam aleikum, Bwana Yesu Asifiwe*; na hata salamu iliyoibuliwa na Rais wa Awamu ya Sita Mhe. Samia Suluhu Hassan: *Ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…Kazi iendelee.* Salamu hizi nyingine hazina utabaka kama ilivyo *shikamoo*; salamu hizo nyingine hutumika sawa iwe mtoto anamsalimia mkubwa au kinyume chake.

Mtazamo hasi mwingine kutoka katika majibu mengine mfano ukichukuliwa kutoka namba 8 katika Jedwali Na. 2 ni kwamba, imebainika wazi kuwa wapo watu wengine hufanya jitihada za kuikwepa kusudi salamu hiyo na kuamua kutumia salamu nyingine. Suala hili lilijidhihirisha waziwazi kutoka katika njia ya ushuhudiaji. Wakati mwingine tulishuhudia watu wengine wakionesha kutotaka kusalimiwa *shikamoo*. Baadhi ya watu wanaonesha kuwa wakisalimiwa salamu hiyo ni kama vile wanazeeshwa.

Kwa hiyo, kutokana na majibu ya watoataarifa hawa, na kwa kuongozwa na EM, ni dhahairi kwamba kiasi kikubwa cha watu wanaridhika na kupendezwa na matumizi ya salamu ya shikamoo. Ijapokuwa salamu hiyo imekubalika na wengi, bado hatuwezi kupuuza moja kwa moja mtazamo wa wanaoikataa hasa ukizingatia kwamba waliodai kukubaliana na salamu hiyo si asilimia kubwa sana (51%); hii ina maana kwamba bado kiasi cha watu wa kutosha tu kinaona salamu hiyo si nzuri. Aidha, tunaona hata baadhi ya sababu ambazo wanazitoa wanaodai salamu hiyo ni mbaya zina mashiko. Mfano wa sababu zenye mashiko za watu wanaoona salamu hiyo si nzuri ni: asili ya salamu hiyo ni ya kikoloni, salamu ya kiutabaka na salamu hiyo haina mwendelezo wa kuweza kujua hali ya mtu ipoje (nzuri, anaumwa, n.k). Suala hili linalandana na utafiti wa Mapunda na Sommer (2017) waliotafiti matumizi ya *shikamoo* katika jamii ywa Wangoni. Pamoja na mambo mengine, ilibanika kwamba licha ya wazee kuwalaumu vijana kutumia *shikamoo* wanapozungumza Kingoni, bado vijana hao walidai hawawezi kuacha kwa sababu wanakwenda na wakati. Vivyo hivyo, wale ambao hawaipendi salamu ya *shikamoo* wasilazimishwe kuipenda kwa kuwa wana sababu za msingi za kutoipenda. Suala hili linashadidiwa na EM ambayo inasisitiza kuwa mawasiliano si hisabati, yanaweza kubadilika kulingana na utamaduni pamoja na mazingira.

## 5.0 Hitimisho na Mapendekezo

Makala haya yameeleza asili ya salamu ya *shikamoo* ni maneno "*nashika miguu*". Ni salamu ambayo wakati inaanza kutumika ilihusisha watwana kusalimia mabwana wao. Kwa hiyo, ni ukweli usio na shaka kwamba asili ya salamu hiyo inanasibishwa na masuala ya utumwa na ukoloni. Aidha, ni dhahiri kwamba salamu hii kwa sasa kama ambavyo imesanifishwa na miongozo ya Kiswahili sanifu inachukuliwa kuwa ni salamu ya heshima ambayo mara nyingi hutumiwa na mtu mdogo kiumri kumsalimia mtu mkubwa kiumri. Licha ya asilimia kubwa ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili kuwa na mtazamo chanya na salamu ya *shikamoo*, bado kuna watu japo si wengi ukilinganisha na wenye mtazamo chanya, wana mtazamo hasi na salamu hiyo. Kuna sababu nne zinazotolewa kuhusu salamu hiyo kuwa na changamoto au mtazamo hasi. Sababu ya kwanza ni salamu inayonasibishwa na ukoloni. Sababu ya pili, ni salamu inayohusudu matabaka tofauti na salamu za kiimani (Bwana Yesu asifiwe, salaam aleikum), salamu za kawaida (habari za asubuhi/mchana/jioni), au salamu mpya ya Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan (ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania… kazi iendelee!). Sababu ya tatu, salamu hiyo haina mwendelezo wa kuweza kujua hali ya mtu ipoje (nzuri, anaumwa, n.k). Aidha, kwa kuzingatia Nadharia ya EM inayojikita katika suala la mawasiliano, miongoni mwa watu na

utamaduni pamoja na mazingira yao, hatuwezi kupuuza mapokeo hasi ya salamu hiyo hata kama ni watu wachache kuliko waliopokea kwa namna chanya.

Ijapokuwa si suala rahisi kuielekeza jamii jinsi ya kutumia lugha, yaani kutumia mkabala elekezi wa uchambuzi wa lugha, ni vema kuweka wazi masuala yenye mantiki ambayo kwa namna moja au nyingine jamii inaonekana kukengeuka. Mathalani, tukitoa mfano mwingine tu tofauti na mjadala husika katika makala haya ili kueleza umuhimu wa jambo hili; baadhi ya watumiaji wa lugha katika miktadha rasmi wanakosea uandishi na/au utamkaji wa baadhi ya maneno au virai, na limekuwa kama ni jambo la kawaida. Baadhi ya virai au maneno yanayokosewa ni: *dhalura* badala ya ***dharura***, *kwasababu* badala ya ***kwa sababu***, *waatakao fika* badala ya ***watakaofika***, *wamehairisha* badala ya ***wameahirisha.*** Kwa hiyo, kwa kuwa uandishi huu wa kimakosa umetamalaki miongoni mwa waandishi wa nyaraka na habari rasmi, hatuwezi kuamua kuacha tu kwa kigezo kwamba jamii ndiyo inayoamua itumie vipi lugha. Kwa kuzingatia suala la muktadha na mazingira ya matumizi ya lugha ambayo ni mukdha rasmi, ni lazima utolewe mwongozo wa kurekebisha hali hiyo. Vivyo hivyo, katika jambo hili tunalolijadili katika makala haya, endapo imebainika wazi kuna ukengeushi wa mambo, yanatakiwa kunyooshwa vema bila kujali yatafuatwa na watumiaji ama la. Kwa hiyo, katika hili la matumizi ya *shikamoo;* kwa kuwa salamu hiyo ina mapokeo tofautitofauti, wapo wanaoiona salamu hiyo ni nzuri na wapo wanaoona salamu hiyo si nzuri (bila kujali ni wachache), ni vema sasa salamu hiyo isilazimishwe kutumika bali kila mmoja aeleweshwe asili au/na historia pamoja na mantiki ya salamu hiyo kisha mtu mwenyewe amue kuchagua kusalimia kwa kutumia *shikamoo* au atumie salamu nyingine. Pendekezo hili halina shida kwa sababu zipo pia salamu nyingine tofauti na shikamoo katika lugha ya Kiswahili kama vile habari za asubuhi/mchana/jioni/usiku/za siku, unaendeleaje, salamu za kiimani, na hata ile salamu ya hivi karibuni (mwaka 2020) hususani kwa Watanzania iliyotolewa na Rais wao, Samia Suluhu Hassan: *ninawasalimia kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania….na kazi iendelee.*

Aidha, huku tukifahamu kuwa kila lugha ina utamaduni wake, lakini si dhambi kuhusisha lugha moja na nyingine. Tunafahamu kuwa lugha ya Kiingereza ni moja ya lugha zinazotumika sambamba na Kiswahili, na mara kwa mara nyaraka za lugha moja kati yake hutakiwa kutafsiriwa katika lugha nyingine. Swali; je, salamu ya *shikamoo* inatafsiriwa vipi katika lugha ya Kiingereza? Swali hili ni gumu na wazuoni wengi wataishia kusema kwamba Kiswahili na Kiingereza ni lugha zenye tamaduni tofauti. Licha ya jibu hilo kuwa na mantiki, bado tunaona salamu nyingine kama vile habari za asubuhi zinapata tafsiri kirahisi na mwafaka tu katika lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, kwa kuwa lugha hizo mbili (Kiswahili na Kiingereza) hutumika sambamba kama ambavyo imeelezwa, ni dhahiri kwamba inapokuja suala la kupata tafsiri ya s*hikamoo* kwa lugha ya Kiingereza inakuwa ni changamoto, ijapokuwa inawezekana; ndiyo maana makala haya yanapendekeza watu kutolazimishwa kutumia salamu hiyo kwa sababu baadhi ya watu wana mapokeo hasi ya salamu hiyo na wana uwezo wa kutetea kimantiki mapokeo hayo hasi.

## Marejeleo

Brown, P. (1980): "How and why women are more polite. Some evidence from a Ma-yan community". In: McConell-Ginet et al. (eds.): Women and language in literature and society. New York, Praeger: 111–136.

Mapunda, G na Sommer, G (2017). When Shikamoo Mama/Baba replaces Tukuwoni Mawu/Dadi: An account of shifting access rituals among the Ngoni of Tanzania. *Linguistik Online*, 84(5): 63-90. Inapatikana katika https://doi.org/10.13092/lo.84.3847

Hymes, D. H. (1972). "Models for the interaction of language and social life". In J. J. Gumperz & D.H. Hymes (Eds.), Directions in sociolinguistics: The Ethnography of Communication (35–71). New York: Holt, Rinehart and Winston.

Hymes, D.H. (1974). *Foundations in Sociolinguistics: An Ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Hymes, D.H. (1975). "Breakthrough into Performance". Katika D. Ben-Amos & K. S. Goldstein (Wah.) *Folklore: Performance and Communication* Kur. 11–74.The Hague: Mouton

Philipsen, G. (1987). 'The prospect for cultural communication'. Katka K. Lawrence (Wah.), Communication theory: Eastern and Western perspectives Kur. 245–254. New York: Academic Press.

Schegloff, E.A. (1968). Sequencing in conversational openings. *American Anthro-`pologist*, 70 (6): 1075–1095.

Yahya-Othman, S. (1995). Aren't you going to greet me? Impoliteness in Swahili greet-ings. *Text*, 15(2): 209–227.

William, D. (2018). Matumizi ya Neno "Shikamoo" katika Mtandao wa *Jamiiforums*: Uchunguzi wa Maana yake Kimuktadha. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.